# KUKUBALIWA KATIKA HOSPITALI KWA AMRI YA HOSPITALI ILIYO NA VIZUIZI

(Sehemu ya 37 na 41 ya Sheria ya Afya ya Akili 1983)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la Mgonjwa | |
| 2. Jina la mtu anayesimamia utunzaji wako (“daktari wako anayewajibika”) | |
| 3. Jina la hospitali na wadi | |
| 4. Tarehe yako ya agizo la hospitali | |

## Je! ni kwanini niko hospitalini?

Unawekwa katika hospitali hii kwa amri ya Korti. Korti imesema unaweza kuwekwa hapa chini ya sehemu ya 37 ya Sheria ya Afya ya Akili 1983.

Hii inaitwa “amri ya hospitali”. Inamaanisha kuwa madaktari wawili wameelezea Korti kuwa wanafikiria una shida ya akili na kuwa unahitaji kuwekwa hospitalini.

Kwa sababu za usalama wa umaa, Korti pia imekupa amri ya kizuizi chini ya sehemu ya 41 ya Sheria ya Afya.

## Je! amri ya kizuizi ni nini?

Amri ya kizuizi inmaanisha kuwa hauwezi kuruhusiwa kutoka hospitalini isipokuwa Katibu wa Jimbo wa Haki au Mahakama iseme unaweza kutoka, na kutoka kwako kunaweza kuwa juu ya mahsarti fulani ambayo yanaweza kufafanuliwa kwako karibu na wakati huo. Ukiwa hospitalini, mtu anayesimamia utunzaji wako (daktari wako anayewajibika) lazima apate makubaliano ya Katibu wa Jimbo wa Haki kabla uweze kuenda kwa likizo fupi au utumwe katika hoapitali nyingine. Lazima wakuchunguze na watume ripoti kukuhusu kwa Katibu wa Jimbo wa Haki angalau mara moja kwa mwaka.

